

# HUDUMA ZA KUSAIDIA, KUELEKEZA NA KUTATHMINI WATEJA (CUSTOMER ASSISTANCE, REFERRAL & EVALUATION SERVICES, CARES)

HUDUMA ZA KUSAIDIA, KUELEKEZA NA KUTATHMINI WATEJA



## PROGRAMU YA WAJIBU KWA WATEJA (CUSTOMER RESPONSIBILITY PROGRAM, CRP)

Programu ya Wajibu kwa Wateja (CRP) husaidia familia zenye kipato cha chini kulipa bili zao za gesi na kudumisha huduma kwa kuwapa bei nafuu iliyowekwa ya kila mwezi. Kujua bei ya gesi kabla ya wakati kutimia kunaweza kusaidia familia kupanga bajeti kwa matumizi ya boma.

Mbali na kupunguza bili ya kila mwezi, CRP hutoa msamaha wa deni kwa kila mwezi bili hulipwa kikamilifu na kwa wakati. Wanaoshiriki katika program hii wanaweza pia kupata huduma za bure za hali yakuboresha hewa ili kuboresha ufanisi wa nishati nyumbani kwao.

## PGW CARES

PGW iko hapa kukusaidia wakati wako wa shida. Jifunze kuhusu mipango na huduma ambazo zinaweza kukusaidia leo.

Kusanya thibitisho ya mapato kwa kila mtu wa boma (haswa malipo ya kulipia ndani ya siku 30 zilizopita, barua ya usalama wa kijamii) kasha sajili mtandaoni kwa [www.pgworks.com/crp](http://www.pgworks.com/crp). Vinginevyo, unaweza kujusajili kwa kutumia karatasi.

Ikiwa hakuna mtu katika boma aliyepokea aina yoyote ya mapato, msaada wa kifedha, msaada wa watoto, au msaada wa pesa taslimu katika siku 30 zilizopita, lazima ujaze Kauli ya Kutokuwa na Mapato (Statement of No Income). Kauli hiyo inatoa nafasi ya kuelezea jinsi boma yako inakidhi gharama ya chakula, nyumba, na matumizi ya kila mwezi. Kwa habari zaidi piga simu 215-235-1000

### MWONGOZO WA KILA MWEZI WAMALIPO YASIOKATWA KODI

UKUBWA WA BOMA	CRP	Programu Ya Nishati Ya Kusaidia Boma Zenye Upato Wa Chini (Low Income Home Energy Assistance Program, LIHEAP) & CRISIS	Hakiba Ya Huduma Za Haraka Za Matumizi (Utility Emergency Services Fund, UESF)
1	\$1,610	\$1,595	\$1,861
2	\$2,178	\$2,155	\$2,514
3	\$2,745	\$2,715	\$3,168
4	\$3,313	\$3,275	\$3,821
Kila mtu binafsi	\$568	\$560	\$653

## **PESA TASLIMU ZA PROGRAMU YA NISHATI YA KUSAIDIA BOMA ZENYE UPATO WA CHINI (LOW INCOME HOME ENERGY ASSISTANCE PROGRAM, LIHEAP) & MSAADA WA MIGOGORO (CRISIS)**

Programu Ya Nishati Ya Kusaidia Boma Zenye Upato Wa Chini (LIHEAP) ni mpango wa kitaifa unaotoa Msaada wa Fedha na Msaada wa Migogoro kwa familia zenye kipato cha chini. Kiwango cha ruzuku kinategemea ukubwa na mapato ya boma, na kamwe haifai kulipwa. Misaada ya ruzuku ina thamani ya hadi \$1000 na inashughulikia bili za kupasha joto.

Ruzuku ya Msaada wa Migogoro husaidia kuzuia kukatizwa ikiwa mteja ana deni ya zamani, na inarejesha huduma ya gesi ikiwa imekatizwa. LIHEAP kawaida hufunguliwa kati ya mwezi wa Novemba na Aprili, hata hivyo ruzuku maalum wakati mwingine hufanywa mwaka mzima. Omba LIHEAP mtandaoni kwa [www.compass.state.pa.us](http://www.compass.state.pa.us) au ujisaji kwa njia ya ya karatasi. Piga simu kwa 215-235-1000 upate maelezo zaidi.

## **HAKIBA YA HUDUMA ZA HARAKA ZA MATUMIZI (Utility Emergency Services Fund, UESF)**

Hakiba Ya Huduma Za Haraka Za Matumizi (UESF) ni mpango wa ruzuku unaofadhiliwa kibinafsi kusaidia familia zenye kipato cha chini ambazo zinachelewa kulipa bili zao za matumizi. Ili kujisajili, mteja lazima a) awe na bili 1 kamili iliopita na awe na deni ya zamani ya angalau \$30; AU b) awe na ilani ya kukatizwa. UESF imeundwa kulipa deni yote ya bili ya huduma ya mteja aliyeshindwa kulipa. Mbali na kutoa ruzuku za matumizi, UESF inaendeleza mipango kadhaa inayolenga kuleta utulivu wa makazi-tembelea [www.uesfacts.org](http://www.uesfacts.org) kwa maelezo zaidi. Kuomba ruzuku ya UESF, wasiliana na Kituo cha Nishati cha Jirani (Neighborhood Energy Center). Piga simu kwa 215-972-5170 upate maelezo zaidi



## **BAJETI YA NJIA RAHISI**

Wateja wasio na chochote kwenye akaunti zao za PGW wanaweza kujisajili katika Bajeti ya Njia Rahisi. Baada ya kujisajili, PGW inakadiria matumizi yako ya gesi ya kila mwaka na hugawanya jumla kwa kipindi cha miezi 12. Hii inasawazisha malipo kwa kipindi cha mwaka na husaidia familia kutabiri kupasha joto kutagharimu pesa ngapi kila mwezi. Piga simu kwa 215-235-1000 ili kujisajili.

## **MIPANGO YA MALIPO**

Wateja walio na salio kwenye akaunti zao za PGW wanaweza kustahiki Mpangilio wa Malipo wa kulipa deni hiyo wakati wa kipindi maalum. Lengo la mpangilio huu ni kuwapa wateja njia ya kudumisha au kurejesha huduma ya gesi wakati wanapopunguza deni. Piga simu kwa 215-235-1000 upate maelezo zaidi

## **ENERGYSENSE**

EnergySense hutoa punguzo na misaada ya kununua tanuri hita za maji moto zinazotumia nishati ipasavyo nyumbani kwako. Jisajili katika [www.pgwenergysense.com](http://www.pgwenergysense.com). Kwa habari zaidi piga simu kwa 855-749-7658.